

LEARNING BY EAR

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Episode 10: “Tubu kwanza, kisha maridhiano”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

List of characters by scenes:

SCENE ONE: FOREST MEETING BETWEEN TORUBES AND KIMBEBES

- Lawi (m, 20)
- Waliani (m, 75)
- several women break down in tears and wailing (at least 4)
- at least 3 men

SCENE TWO: MATONGE, SOMBA AND KERO ON THE RUN

- Matonge (m, 65)
- Somba (m, 55)
- Kero (f, 55)

SCENE THREE: RITUAL CLEANSING AT A SACRED STREAM

- Waliani (m, 75)
- Mixed crowd (at least 5 ppl)

SCENE FOUR: MATONGE, SOMBA AND KERO FLYING TO THE HAGUE

- **Matonge (m, 65)**
- **Somba (m, 55)**
- **Kero (f, 55)**

SCENE FIVE: MATONGE, SOMBA AND KERO FLYING TO THE HAGUE

- **Waliani (m, 75)**
- **Masambo (m, 50)**
- **Mixed crowd (at least 5 ppl)**

Msimulizi

INTRO:

Hujambo na karibu katika kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha kumi na cha mwisho katika hadithi hii ya mikinzano na utatuzi, kwa jina, “**Palipo na wazee**”. Katika kipindi kilichopita, rais Matonge na wafuasi wake Somba na Kero walipewa mwito kutoka korti ya kimataifa ya mahakama ya ICC. Lakini wakaamuwa kwenda ukimbizini. Kwengineko, jamii mbili za watorube na wakimbebe walikutana ndani ya msitu nyika kujadiliana, na kutafuta msamaha na maridhiano wakiongozwa na mzee Waliani. Wacha tuone leo kutajiri yapi, katika kipindi cha leo kiitwacho, “**Tubu kwanza, kisha maridhiano**”. Tunaanza na kabila hizi mbili ikiwa zimekutana kwa minajili ya maridhiano.

SCENE ONE: FOREST MEETING BETWEEN TORUBES AND KIMBEBES

1. SFX: FOREST AMBIENCE

2. WALIANI: (sings a short sad prayerful song) Mungu wetu, tunakuomba, mababu zetu, tunawauliza, katika kipindi hiki cha uchungu, maumivu na machozi. Tunaomba muongozo wenu, mutuongoze kwenye njia ya amani, ukweli na maridhiano. Tufungue mioyo yetu, nyimbo na ngoma na zianze!

3. (women humming and dancing and clapping)

4. WALIANI: Sherehe hii itakuwa ndefu, na chungu kwa sababu ya makosa yaliyofanywa, damu isiyo na hatia ilimwagwa, wengi wakawachwa bila makao baada ya nyumba zao kuchomwa. Na kwa mara ya kwanza, ningeliwaomba tukae mduara, sote tuweze kuonana. Kwanza tuwashe moto katikati yetu.

5. SFX: FIRE STARTING TO BURN WITH PAPER AND FIREWOOD

6. WALIANI: Yeyote anayetaka kusamehewa, kutubu na maridhiano, sharti aje karibu na moto, apige magoti, au alale chali kama ishara ya kuungama. Alafu awatake radhi aliwakosea na kuwaomba msamaha vilevile. Alafu tutaendela. Tuendeleeni kuimba huku wanaume wakizisaka nyoyo zao

(Singing continues in background by women)

- 7. LAWI:** (remorseful) Nitaanza, kwa sababu mimi ndiye niliongoza uvamizi, jina langu ni Lawi, nilikuwa mstari wa mbele.
- 8. (several women break down in tears and wailing, then only sobs are left)**
- 9. LAWI:** (also in tears) Kiongozi wenu Dere alichukuwa ng’ombe zetu nyingi, wakati nikiwa malishoni nikilisha ng’ombe za babangu. Niliapa, nikampa ahadi..(pause)
- 10. WALIANI:** Ni sawa, kijana wangu, elezea kila kitu. Toba ya kweli, ndio chanzo cha maridhiano.
- 11. LAWI:** Nilijiapa sitapumzika, mpaka niziregshe ng’ombe za babangu zilizochukuliwa kimabavu. Sasa palipokuja mtu wa serikali na kutupatia bunduki, nilijuwa wakati umewadia. Wakati wa kulipa kisasi umewadia.
- 12. WALIANI:** Unafikiria ni kwanini watorube walipatiwa bunduki? Mumeishi miaka yote bila bunduki! Kweli mulizihitaji? Na swali hilo pia ni lenu, watu wakimbebe. Kumbukeni, silaha zaweza kushinda vita, bila kuleta amani. Endelea Lawi.

- 13. LAWI:** Mara ya kwanza niliposhika bunduki, niliwaza tu kuuu watu wakimbebe. Niliongozwa na chuki, lakini sikunua kuuu au kuumiza mtu yeyote. Niliamuru wenzangu wasiue wale wasio na hatia. Naomba radhi na msamaha. Kwa waume ambao wake zao waliuawa, mama waliopoteza watoto wao, hata watoto waliopoteza wazazi wao. Nisameheni!
- 14. (Crowd responds in a chorus, “Tumekusamehe kwa ajili ya Mungu, na mababu zetu ambao wako nasi”)**
- 15. LAWI:** **(Breaks down in tears)** Asanteni, na shukrani.
- 16. WALIANI:** Ni muhimu kujuwa nani alihusika kufanya nini, haijalishi itakuwa uchungu kiasi gani. Hivyo tu ndio tutajifungua kutoka minyororo ya chuki, hukumu na uchungu. Tutakuwa hapa kwa muda, kwa hivyo kila mtu achukuwe muda atafakari. **(calls out)** Mwengine!
- 17. MSIMULIZI:** Mmoja baada ya mwengine, wale waliohusika kuuu na maasi mengine walijitokeza na kutubia, wakilia, na wengine kwa majuto, walijiziba nyuso zao kwa majivu ya moto ule. Ilikuwa sherehe ya siku nyingi na yenye hisia tofauti. Baada ya watorube, walikuja wakimbebe. Upatanisho wa jamii hizi ulichukuwa wiki mbili, kisha watu wote walikusanyika kujitakasa. Lakini kwanza, tuwawahi kina Matonge, Somba, na Kero. Wanaotakiwa na ICC sasa wakiwa mbioni.

SCENE TWO: MATONGE, SOMBA AND KERO ON THE RUN

18. SFX: TRUCK BEING DRIVEN ON A ROUGH ROAD

19. MATONGE: Bado umbali gani, mpaka tufike mpakani?

20. SOMBA: Tuko karibu, muheshimi....ah nimesahau, wewe siye raisi tena. **(laughs)**

21. KERO: Somba, usiseme hivyo. Matonge alikupa madaraka ya mkuu wa majeshi; unafaa kumshukuru.

22. MATONGE: Kweli mambo yamenigeukia. Dakika moja nilikua ikulu, saa hii niko kwenye gari kebe kama nini, sijulikani naenda wapi!

23. SOMBA: Amini ni bora kuliko aibu ungelipata humu nchini na ulimwenguni kwa jumla kwa ajili ya hii kesi.

24. SFX: BULLETS BEING FIRED FROM SEVERAL GUNS

25. MATONGE: **(terrified)** Kuna nini? Nani anayetupiga risasi?

26. SOMBA: Kanyaga mafuta, Kero! Kero, endesha haraka!

27. SFX: TRUCK DRIVEN FASTER

- 28. KERO:** Najaribu.Nafanya kila niwezalo!
- 29. MATONGE:** **(Breathing heavily)** Somba, Kero, walikuwa kina nani waliokuwa wakipiga risasi gari ya wanajeshi wa serikali?
- 30. SOMBA:** Ni kundi lile jengine tulilolipa silaha msimu wa kura zilizopita.
- 31. MATONGE:** **(shocked)** Ati? Yaani, kwani kila mwananchi anamiliki bunduki humu nchini? Hiyo si italetta vita vya wenyewe kwa wenyewe.
- 32. KERO:** Haswa, ndio maana ni vyema tunatoroka, mambo yameharibika.
- 33. SOMBA:** **(relieved)** Ah sasa, tunakaribia mpakani. Itanibidi niwaambie majeshi yangu yatauchie tupite.
- 34. SFX: TRUCK COMES TO A HALT**

35. MSIMULIZI: Jambo ambalo hawa watatu hawakulijua, ni kwamba punde tu walipotoroka basi msako wao ulianza. Walishikwa na walinda zamu wa mpakani, na wakaregeshwa jijini kwa kosa lakutumia vyeo vyao vibaya, na wakatiwa kizimbani kusubiri hukumu yao mahakamani. Mahakama ya kimataifa pia iliwasubiri. Lakini turudi tena msituni, mtoni ambapo sherehe ya kuwasafisha wakosaji imeanza.

SCENE THREE: RITUAL CLEANSING AT A SACRED STREAM

36. WALIANI: **(praying)** Mababu zetu watukuka, kwa siku nne, tumelia, na kutubu, na hivi ninavyomwaga nafaka hii ya mchele kwenye mto, tunaomba ubaya wote utuepuke. Kama ambavyo hatutauona tena huo mchele. Nasi tusione tena ubaya huo miongoni mwetu.

37. SFX: GRAINS FALLING ON A STREAM

38. WALIANI: Uovu umeshindwa. Watu wote wamejitakasa!

39. SFX: HUGE APPLAUSE AND CELEBRATION FROM GATHERING

40. WALIANI: Sasa, nimetayarisha kinywaji rasmi, ambacho mababu zetu walikiita “Dawa Chungu”. Itaburudisha “mioyo yenu” na kuwaunganisha pamoja. **(prays)** Kwa kinywaji hiki, nawauliza babu zetu mutuondolee chuki yote, na muitulize mioyo ya watu wetu. Naomba muwaunganishe, waishi kwa upendo.

41. SFX: SEVERAL PEOPLE SIPPING FROM A DRINK, ONE AFTER THE OTHER (studio)

42. MSIMULIZI: Wahini na wahiniwa wote walikunywa kinywaji hicho. Hatimae wakati wa kwenda ICC, uliwadia, kwa Somba, Matonge na Kero. Wote walikaa katika ndege wakielekea Hague, wakiwa chini ya ulinzi mkali na mikononi wamefungwa pingu.

SCENE FOUR: MATONGE, SOMBA AND KERO FLYING TO THE HAGUE

43. SFX: SIGNAL FOR UNFASTENING SEAT BELTS/inside plane atmo

(Announcement to unfasten seat belt because plane has reached cruising altitude)

44. MATONGE: **(Annoyed)** Ala! Yani ulitaka tujifunge mikanda ya usalama na mikono yetu ina pingu? Nilikuwa Rais usisahau!

45. SOMBA: Mimi pia!

46. MATONGE: Hukuwa Rais Somba, Ni mimi!

47. SOMBA: Nilikuwa nazungumzia mikanda ya usalama.

48. KERO: Hebu nyamazeni, tulieni na mufurahie safari ya ndege. Huwenda ikawa safari yenu ya mwisho kwa ndege.

49. MATONGE: Kwanini? Nina hakika nitapatikana sina hatia.

50. KERO: **(sarcastic laugh)** Ikiwa huna hatia, basi mimi ni mkuu wa dini haswa! Kifungo cha maisha kinatukodolea macho sote.

51. MSIMULIZI: Jambo moja la ukweli. Hakuna kosa lisilo hukumu, au lisilopatanishika. Kule msituni, watu wengi waliamuwa kuregesha silaha, na mlima wa silaha mbali mbali ukaibuka. Waliani alikuwa karibu kumaliza mkutano wake.

SCENE FIVE: LIBATIONS FOR THE ANCESTORS IN THE FOREST

52. WALIANI: Tukikaribia kumaliza sherehe yetu. Wakati umewadia wa kuchinja mnyama huyu na kuregesha shukrani kwa mababu zetu. Kuwashukuru kwa kuwa nasi, na tuwaulize wazilinde hizi kabila mbili ambazo zimepatana leo hii.

53. MASAMBO: Mzee Waliani, yote yaliyotendeka yamenifunza. Mara mbili sasa, tumepata maridhiano kupitia kwa wavyele. Kwa hivyo nitapeana mifugo yangu, sio ng’ombe mmoja au wawili lakini watatu! Kwa kazi hii na watu wale!

54. SFX: HUGE APPLAUSE AND CELEBRATION FROM GATHERING

55. WALIANI: Upendavyo Masambo, utakavyo. Natumai huu ni wakati muafaka wa kurudia itikadi za mababu zetu. Kwani walipo na wazee, hapaharibiki jambo!

OUTRO:

Hapo ndio tumeikia mwisho wa hadithi yetu ya mchezo huu wa kuigiza redioni, kupitia kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako. Mchezo huu umetungwa na Chrispin Mwakideu. Natumai umefurahia.

Jiunge nasi, kwa kutembelea tovuti yetu www.dw-world.de/lbe. ili kusikiliza, kutupa maoni na kujifunza zaidi. Mpaka tutakapokutana tena, dumisha amani daima.